


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAISI TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



S.L.P295,

IGUNGA

0622 499310 /0764 722625

SHULE YA SEKONDARI IGOWEKO

Kumb Na...S4080/ADM/VOL 1/2021

MZAZI/MLEZI WA .....

SHULE YA MSINGI .....

IGUNGA.

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI IGOWEKO KIDATO CHA KWANZA 2021**

Ninafurahi kukutaarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na **kidato cha kwanza** katika shule hii

Mwaka 2021. Shule ipo umbali wa Km sita (7) Mashariki mwa Simbo, Barabara toka Simbo kwenda Mpyagula inapita hapa. Shule ya sekondari Igoweke ni ya kutwa. Hivyo mzazi / Mlezi atawajibika Kumtafutia Mwanee malazi pamoja na chakula wakati wote akiwa shuleni. Wasichana watapata nafasi ya **HOSTEL** na Mzazi atachangia chakula.

Shule itafunguliwa tarehe **11, Januari 2021** Mwanafunzi atatakiwa kuripoti tarehe hiyo. Aidha mwisho wa kuripoti tarehe **29 Januari 2021**. Mzazi / mlezi atakayechelewa kumleta Mwanafunzi zaidi ya tarehe tajwa hapo juu atachukuliwa Hatua **KALI** za kisheria kwa kukiuka agizo halali la Serikali.

**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**A)Sare za Shule**

**I. WASICHANA**

- ✓ Sketi mbili dark blue nzito yenye marinda ya kupanga yenye marinda na urefu mpaka kwenye kongo mbili.
- ✓ Mashati mawili nyeupe tetroni mikono mifupi
- ✓ Sketi ya damu ya damu mzee nzito kwa ajili ya kazi za nje yenye marinda ya kupanga na urefu mpaka kwenye kongo mbili.
- ✓ Viatu vyeusi vya ngozi visivyo na urembo wala visigino virefu na vyenye kufunga kamba (gidamu)
- ✓ Soksi ndefu nyeupe (stockings)jozi mbili.
- ✓ Sweta la blue la kuvaa wakati wa baridi.
- ✓ Wasichana wa kiislamu wanaruhusiwa kuvaa **HIJABU** (iwe ya rangi nyeupe na isiwena urembo)
- ✓ Jezi moja kwa ajili ya michezo rangi nyekundu au blue (track suit)
- ✓ Viatu vya michezo raba au njumu
- ✓ Begi jeusi la kubebea madaftari

**II. WAVULANA**

- ✓ Suruali mbili za Dark blue nzito zenye mashono ya kawaida suruali iliyobana chini haitaruhusiwa

- ✓ Mashati mawili meupe ya tetroni mikono mifupi
- ✓ Suruari ya damu ya mzee nzito kwa ajili ya kazi za nje yenye mshono wa kawaida kama 1 juu
- ✓ Viatu vyeusi vya ngozi visivyo na urembo wala visigino virefu vyenye kufunga kamba gidamu
- ✓ Soksi ndefu za kaki stockings jozi mbili
- ✓ Sweta la blue la kuvaa wakati wa baridi
- ✓ Jezi moja kwa ajili ya michezo rangi nyekundu au blue (track suit)
- ✓ Viatu vya michezo raba au njumu
- ✓ Begi jeusi la kubebea madaftari

**NB: VITU VYOTE HIVI VITAKAGULIWA**

#### **MAHITAJI YA DARASANI**

- Madaftari makubwa kumi na moja
- Kalamu, penseli, rula na mkebe (mathematical instruments)
- Begi jeusi la kuwekea madaftari na vitabu (ni lazima mwanafunzi awe na begi imara kwani shule itampa vitabu na anapaswa kuvitunza humo)

#### **MAHITAJI YA CHAKULA**

Shule ya sekondari Igoweke inatoa huduma ya chakula kwa wanafunzi wote wanaokaa hosteli na wale wa kutwa kutokana na michango ya wazazi .

#### **KWA WANAFUNZI WA HOSTELI (wasichana wote)**

1. Mahindi debe 6 kwa mwaka au madebe 3 kwa muhula
2. Mchele Kg 40 kwa mwaka au Kg20 kwa muhula
3. Sukari Kg6 kwa mwaka au Kg3 kwa muhula
4. Mafuta lita 6 kwa mwaka au lita 3 kwa muhula
5. Maharage Kg32 kwa mwaka au Kg 16 kwa muhula
6. Fedha ya mpishi, kusaga na chumvi Tshs. 30,000/=

#### **KWA WANAFUNZI WA KUTWA (WAVULANA WOTE)**

1. Mahindi kilo 48 kw mwaka au kilo 24 kwa muhula
2. Mchele kilo 10 kwa mwaka au kilo 5 kwa muhula
3. Maharage kilo 12 kwamwaka au kilo 6 kwamuhula
4. Sukari kilo 4 kwa mwaka au kilo 2 kwa muhula
5. Mafutalita 4 kwa mwaka au lita 2 kwamuhula
6. Fedha ya mpishi Tshs. 15,000/=

Kila mzazi /mlezi ni lazima amkatie mwanafunzi(mwanae) kadi ya **C.H.F** katika za hanati ya Uswaya na sivinginevyo. Huduma ya **C.H.F** hugarimu **Tshs. 5000/=** kwa mwaka (shule haitapokea fedha hiyo ni wajibu wa mzazi/mlezi kuipeleka zahanati).

#### **01. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE**

- a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
- b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shuleni lazima
- c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
- d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
- e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka ya shule wakati wowote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.

- g) Kuva sare za shule wakati wote unapotakiwa.
- h) Kuzingatia ratiba za shule wakati wote.
- i) Kutunza mali za umma.
- j) Itakuwa ni kosa mwanafunzi kukwepa majaribio na mitihani

**02. SEHEMU ZILIZOKATAZWA.**

- a) Guest house na kumbi za starehe
- b) Sehemu za kuuzia pombe
- c) Nyumba za walimu –isipokua kwa kibali
- d) Ofisi za walimu –isipokua kwa kibali tu

**03. MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.**

- i. Wizi
- ii. Uasherati ,ubakaji,ushoga, ulawiti na usagaji.
- iii. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya ,biashara ya madawa yote ya kulevya
- iv. Makosa mengine ya jinai.
- v. Kupigana au kupiga mwanafunzi mwenzake au mtumishi.
- vi. Kuharibu mali ya umma na ya watu wengine
- vii. Kudharau bendera ya Taifa ,picha za viongozi wa taifa,Nembo ya taifa, na fedha za taifa.
- viii. Kuo au kuolewa
- ix. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
- x. Kutoa au kushawishi kutoa mimba
- xi. Kugoma au kuchochea ,nakuongoza au kuvuruga amani na usalama wa watu shuleni.
- xii. Kukataa adhabu halali
- xiii. Kujiachisha shule mwenyewe
- xiv. Kumiliki simu ya mkononi

***KARIBU SANA IGOWEKO SEKONDARI***

.....  
**MKUU WA SHULE**

# IGUNGA DISTRICT COUNCIL

IGOWEKO SECONDARY SCHOOL

P.O.BOX 295,

IGUNGA

Date.....

Ref.No:.....

The Medical Officer (Government Hospital)

.....

.....

## PART A:REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION.

Mr/Mrs/Miss..... (Name in full)

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full time secondary education .The examination should include the following ineligible incase of a defect. Pregnancy (Category 4) will also render a girl ineligible for a secondary education.

1.(a)Eye sight(b)speech(c)Hearing(d)Limb(e)Venereal Deceases (f)Lepresy (g)Epilepsy.

## PART B:MEDICAL CERTIFICATE

(a)Eye sight.....

(a)Hearing.....

(c)Seepch.....

(d)Limb .....

(e)Venereal Deceases.....

(f)Leprosy.....

(g)Epilepsy.....

2. Neuroses .....

3. Other serious deceases.....

4. Pregnancy.....

I have examined the above named and consider that he/she is physically fit/unfit for a full –time secondary education.

Designation.....Date.....

**Signature & Official Stamp**

To be completed by a government Officer)

NB:Incase of any serious health problem(s), the records from the

Government Hospital must be submitted to school while reporting.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA IGUNGA

ANWANI YA MZAZI/ MLEZI

.....  
.....  
.....

HATI YA KUKUBALI MASHARTI KUHUSU MTOTO WANGU KUSOMA SHULE YA SEKONDARI YA KUTWA IGOWEKO.

Mimi.....Mzazi/Mlezi wa

Mwanafunzi.....aliyekua akisoma shule ya msingi

.....iliyoko katika Wilaya ya.....kwa kuzingatia masharti yafuatayo:-

1. Kwamba mtoto wangu atahudhuria masomo kama kawaida nakufanya shughuli zote za kishule akikaa nyumbani/katika nyumba ya kupanga tangu kidato cha 1 hadi cha 4.
2. Kwamba mtoto wangu nitamtimia mahitaji yote kama yalivyo ainishwa katika fomu maalumu ya maagizo ya kujiunga na shule ya kutwa ya Igoweke kwa ukamilifu.
3. Kwamba kwa muda wote huo wote wa miaka minne sitajaribu kabisa kumsumbua Afisa Elimu Mkoa/Wizara kutafuta nafasi ya bweni au hosteli bila sababu muhimu.
4. Kwamba mtoto wangu atafuata sheria na kanuni zote za shule wakati wote wa masomo yake kama zilivyo ainishwa katika fomu ya maagizo ya kujiunga na shule.

.....  
**Sahihi ya Mzazi/Mlezi.**

Namba ya mtihani.....Jinsia.....

## SEHEMU B:-MWANAFUNZI

Mimi ..... Wa shule ya msingi .....ninakubali kujiunga na shule ya sekondari Igoweke na nitafuata masharti yote na sheria zote za shule.

**SAINI**..... **TAREHE**.....

